

Katika kuadhimisha miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tangu ziungane mwaka 1964 mwezi April 26 Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kupitia mradi wa TASAF imezindua matumizi ya barabara za jamii kijiji cha Ntomoko kata ya Haubi kati ya miradi 83 iliyoibuliwa na jamii ikiwemo miradi 53 ya barabara za jamii ambapo utekelezaji wake umefanywa na walengwa kaya 6482 na mgeni rasmi alikua Mh Mkuu wa wilaya ya kondoa Dkt Khamis Mkanachi.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya jamii ya ajira za muda ,Mratibu wa TASAF halmashauri ya wilaya ya kondoa Ndg Donald Somi Jidayi, amesema TASAF imekua na sehemu ya utoaji wa ajira za muda kwa walengwa wenye uwezo kufanya kazi kuanzia miaka 18 hadi 65 kushiriki miradi ya kutekelezwa kwa nguvu kazi za walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF kwa lengo la kuongeza kipato, ujuzi kwa kaya na rasilimali itakayotumika kusaidia jamii nzima kijijini.

“kijiji cha Ntomoko walengwa wametengeneza barabara za jamii kilomota 2.8 kwa ajili ya kuunganisha taasisi kwa taasisi vitongoji kwa vitongoji na vijiji jirani, kila mnufaika wa TASAF hupata ujira wa shilingi 3000/=kwa siku nahii ni baada ya mlengwa kukamilisha kipimo chake alichopewa na taarifa zake kurekodiwa kwenye daftari maalum la mahudhurio kazini yaani JOB ameongeza Ndg Jidayi.

“Katika miradi 83 ya jamii ilikua na bajeti ya sh Bil 1.166 iliyoidhinishwa Na TASAF makao makuu na kutekelezwa katika vijiji vyote 84 ndani ya halmashauri ya wilaya ya kondoa na zoezi la malipo kwa wanufaika kuanza kulipwa stahiki za ujira wa miradi hiyo malipo yatafanyika mwezi Mei kwa vijiji 16 ikiwemo Ntomoko kwa mara ya kwanza na vijiji vilivyobaki kwa mara ya Pili na Juni 2023 kwa awamu mbili ” ameongeza ndugu Jidayi.

Kwa upande wake Mgeni rasmi Mkuu wa wilaya Mh Dkt Khamis Mkanachi amepongeza jitihada za Serikali kutenga fedha Bil 1.166 kupitia TASAF kwa wanufaika walioshiriki kazi 6482 katika halmashauri ya wilaya kondoa ikiwemo wakazi wa kijiji cha Ntomoko kupitia miradi mbalimbali ya ajira ya muda TASAF.

Hafla hiyo ya ufunguzi wa barabara za jamii imeambatana na shamrashamra za Maadhimisho ya miaka 59 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar yenye kuadhimishwa kila ifikapo tarehe 26 april kila mwaka.

Habari na chanzo chetu www.kondoadc.go.tz.